BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 20 Septemba, 2024**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **TAARIFA YA SPIKA:**

II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

III. **MASWALI:**

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

225. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Maeneo ya shehia ya Banda Kuu katika jimbo la Nungwi bado yanaendelea kuathirika na mabadiliko ya tabianchi kutokana na kuendelea kwa hali ya mmong'onyoko wa fukwe wakati wa majira ya Kiangazi.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuzuia mmong'onyoko huo na kuzinusuru nyumba za wakaazi wa maeneo hayo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

35. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Sekta ya Habari ni sekta nyeti na muhimu kwa taifa lolote.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuwaongezea thamani Waandishi wa Habari hapa nchini.

113. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kauli mbiu ya mwaka huu katika kuadhimisha siku ya Kiswahili Duniani ilikuwa ni Kiswahili, Elimu na Utamaduni wa Amani.

Kwa kuzingatia muktadha wa kauli mbiu hiyo, je, kwa kiasi gani jitihada za kuzidi kukieneza Kiswahili duniani zinakwenda sambamba na kuueneza na kuutambulisha utamaduni wa Mzanzibari.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

2. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Inaaminika kuwa wazazi walio wengi hawana mashirikiano ya kutosha na walimu mashuleni, hali inayorudisha nyuma maendeleo ya wanafunzi siku hadi siku.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inaifahamu changamoto hii.

(b) Ni ipi mikakati ya Serikali na Wizara kwa ujumla katika kuimarisha na kuendeleza mashirikiano hayo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

117. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto:

(a) Ni kesi ngapi zenye mnasaba na matatizo ya udhalilishaji kwa watu wazima (wazee) zimeripotiwa kwa mwaka 2021 hadi 2024.

(b) Wazee wengi wamekuwa wakitengwa na kujisikia wapweke. Je, ni zipi jitihada za Serikali za kuona kwamba wazee wanaishi maisha ya furaha na amani.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

54. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini iko vipi juu ya mashirikiano ya 'Tanzania Agricultural Research Institute' (TARI) na 'Zanzibar Agricultural Research Institute' (ZARI) katika kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo ikiwemo uzalishaji wa mbegu asilia za mazao tofauti.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

91. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni tumeshuhudia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akifungua rasmi tukio kubwa la kihistoria la ufunguzi wa bohari mpya ya gesi.

Je, ni kwa kiasi gani wananchi wa Zanzibar watanufaika na kupata unafuu wa matumizi na ununuzi wa gesi kwa bei muafaka.

**Wizara ya Afya:**

77. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Takwimu zinaonesha kwamba mtu mmoja kati ya watu wanne wapo hatarini kupata tatizo la ugonjwa wa kiharusi.

(a) Tathmini iko vipi kwa sasa juu ya ongezeko la ugonjwa huo.

(b) Je, kuna ukweli wowote kwamba vijana unaoanzia umri wa miaka 25 ndio waathirika zaidi wa ugonjwa wa kiharusi.

(c) Kwa sasa tathmini iko vipi juu ya uwepo wa madaktari bingwa wa tatizo hili.

230. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Chukwani ni miongoni mwa vituo vinavyotoa huduma masaa ishirini na nne lakini kwa masikitiko makubwa, kuna uhaba mkubwa wa vitendea kazi na hakuna madaktari kwa muda wote.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuzitatua changamoto hizo.

(b) Je, ni lini Serikali itaipatia ufumbuzi changamoto ya uhaba wa vitendea kazi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

72. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Je, maonesho ya ‘Zanzibar Investment and Tourism Show’ yanatarajiwa kugharimu kiasi gani cha fedha za kitanzania kwa ujumla wake.

(b) Wafadhili, wahisani na wawekezaji wangapi na wepi waliojitokeza katika kufanikisha maonesho haya yanayotarajiwa kufanyika mwezi wa Oktoba, 2024.

(c) Ni yepi matarajio ya ongezeko la watalii kutoka mataifa ambayo kwa sasa bado hayajafungua masoko mapya ya utalii kupitia maonesho haya.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

98. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumlinda mlaji ni jukumu miongoni mwa majukumu ya msingi kabisa ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)

(a) Tathmini iko vipi kwa ZBS juu ya uwepo wa vifaa vyenye teknolojia bora na za kisasa za uchunguzi wa bidhaa mbali mbali za vyakula.

(b) Kwa kiasi gani ZBS inapambana na tatizo la sumukuvu katika utekelezaji wa majukumu yake kupitia bidhaa mbali mbali za vyakula kutoka nje na vile vilivyomo ndani ya nchi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Afya:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**20 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**